

MKATABA WA UCHANGIAJI WA GHARAMA ZA MATUMIZI YA JENGO

Mkataba huu utanza kutumika rasmi tarehe 1 August 2023.

KATI YA

AFISA MADINI MKAZI WA MBEYA S.L.P. 760, MBEYA ambaye atajulikana kama **“mpangishaji”** kwa upande mmoja.

NA

OHDL MINES PRIVATE CO. LTD S.L.P 260, MBEYA , ambaye atajulikana kama **“mpangaji”** kwa upande mwingine.

AMBAPO MPANGISHAJI ni mmiliki wa jengo la ghorofa tano lililoko katika kitalu Na. F kiwanja Na. 13 katika mtaa wa Highland, ndani ya Jiji la Mbeya na ana nia ya kupangisha ghorofa ya pili katika jengo hilo.

NA AMBAPO MPANGAJI ni KAMPUNI YA UNUNUZI NA UZAJI WA DHAHABU yenye nia ya kupanga chumba kimoja katika ghorofa ya pili kwa matumizi ya ofisi pekee.

HIVYO BASI, PANDE ZOTE ZINAKUBALIANA YAFUATAYO:

1. Mpangaji atachangia gharama za matumizi ambazo ni umeme, maji, ulinzi na usafi kwa kiasi kisichopungua shilingi laki moja na nusu (150,000/= kwa mwezi.
2. Kwamba mpangaji atahakikisha jengo hilo linatunzwa muda wote na kuwa katika hali nzuri.
3. Mpangaji hatafanya marekebisho ya kudumu katika jengo hilo bila ya kupata kibali cha maandishi toka kwa mpangishaji.
4. Kwamba pande zote mbili zitakaa na kufanya marejeo (*review*) pindi kutakapokuwa na haja ya kufanya hivyo.
5. Masharti ya mkataba huu yatabadilishwa kwa pande zote mbili kukaa pamoja na kufanya marejeo.

6. Kwamba upande wowote unaokusudia kuvunja mkataba huu utatoa notisi ya miezi sita kwa upande mwingine kabla ya kuvunjwa kwa mkataba.

**KWA KUSHUHUDIA MKATABA HUU PANDE HUSIKA ZINAWEKA SAINI
KAMA IFUATAVYO:-**

IMESAINIWA NA Atilio Simoni
M. Bwana KYN

AMBAYE NI AFISA MADINI MKAZI
MKOA WA MBEYA leo tarehe 24 August 2023.



MPANGISHAJI

Mining Commission
P.O. BOX 760
MBEYA

IMESAINIWA NA BENIS DANIEL JACKSON
MKURUGENZI WA KAMPUNI YA OHDL MINES LTD
.....
MKOA WA MBEYA leo tarehe 24 August, 2023



MPANGAJI

OHDL MINES PRIVATE LIMITED
DIRECTOR